# JARIDA LA RS RUVUMA







## TOLEO LA JULAI 2024



# KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA MWEZI JULAI 2024

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

## YALIYOMO

1.Tamasha la utamaduni la kitaifa kufanyika Songea

2.Serikali ilivyowakomboa wananchi wa Mpitimbi

3.Bwawa la Mpitimbi kivutio kipya i

4.Serikali yaiboresha hospitali ya Tunduru

5.Robo tatu ya Wilaya ya Namtumbo ni hifadhi

6.Ndumbaro alivyosikiliza kero za wananchi

7.Serikali yatoa bilioni 1.77 kujenga shule Mbinga

8.Wananchi Madaba waaswa kufuga nyuki

9.Wanafunzi kidato cha sita waahidi kufanya vizuri

10.Wazazi wahimizwa kutoa mlo kamili kwa wanafunzi

11.Wizara yakabidhi gari la TANESCO Mbinga

12.Ukumbi wa kisasa sekondari ya Samia Namtumbo

13.Vijiji 84 Nyasa vyapewa umeme

14.Waziri Kapinga agawa gesi kwa wananchi Mbinga

15.Mbunge Namtumbo akabidhi mitunge 300 ya gesi

16.Waziri azindua kampeni ya kitaifa ya matumizi sahihi ya mbolea

17.Maagizo ya Waziri Mkuu kwa wakuu wa mikoa na wilaya

18.Barabara ya Mbinga – Mbambabay yageuka kivutio

19.Nyumba ya Nyerere na Samora kivutio cha utalii

20.Wananchi waomba Wilaya ya Namtumbo igawanywe

21.Fursa nyingine ya utalii Nyasa

22.Wananchi Namtumbo waomba huduma za kibingwa

23.Wagonjwa 496 Namtumbo wagundulika na pressure

24.Askari TANAPA wapiga kambi kukabiliana na wanyama waharibifu

25.Kaya 400 Tunduru kufaidika na mradi wa umwagiliaji

26.Wafanya biashara wa mazao Mbinga watahadharisha

27.Milioni 120 za mapato ya ndani zajenga wodi tatu Mbinga

28.Watumishi wapya 675 Ruvuma hawajafanyiwa upekuzi

29.Tunduru yapata Hati Safi miaka mitano mfululizo

30.Kahawa inayovutia zaidi Duniani ipo Nyasa
31.Siri ya Halmashauri zote Ruvuma kupata Hati Safi
32.Mbinga DC yaongoza ukusanyaji mapato
33.Madaba yajivunia Hati Safi
34.Muonekano wa Kituo cha Afya Kihagara
35.Nyasa bado ni kitovu cha utalii Ruvuma
36.Kaya zaidi ya 18,000 Ruvuma zahitimu TASAF
37.RC Ruvuma aagiiza udhibiti upotevu wa fedha
38.Mfumo wa M.Mama kushuka hadi ngazi ya jamii
39.RC Ruvuma awakabidhi wakuu wa wilaya magari mapya
40.Mkoa wa Ruvuma wapata Tuzo nyingine
41.Kisiwa cha Puulu kilivyosheheni vivutio vya utalii
42.Bilioni 2.5 zajenga hospitali Mbinga
43.Hospitali ya Namtumbo kuchunguza magonjwa ya moyo
44.Muonekano wa hospitali ya Wilaya ya Nyasa
45.Bilioni 3.7 zilivyojenga majengo 16 hospitali ya Madaba
46.Utamaduni unavyochochea maendeleo Ruvuma
47.Ifahamu hifadhi ya Gesimasoa
48.Makala ya tabia ya sokwe inafavyonana na binadamu kwa asilimia 98

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.

Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## TAMASHA LA UTAMADUNI LA KITAIFA KUFANYIKA AGOSTI UWANJA WA MAJIMAJI SONGEA



TAMASHA la Utamaduni la Kitaifa la tatu linatarajia kufanyika kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma  mwezi Agosti mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tamasha hilo Joel Mbewa amesema tamasha la kwanza la  kitaifa la utamaduni lilifanyika mkoani Dar es salaam mwaka 2022 na tamasha la pili lilifanyika mkoani Njombe mwaka 2023.

Amesema katika matamasha hayo mawili ya kitaifa Mkoa wa Ruvuma ulifanikiwa kushika nafasi ya sita kitaifa kati ya mikoa 31 ya Tanzania Bara na visiwani.

“Kwa kuwa tamasha hili mwaka huu kitaifa linafanyika mkoani Ruvuma,tumedhamiria kufanya vizuri Zaidi ikiwezekana kushika nafasi ya kwanza kitaifa kati ya mikoa 31 inayoshiriki kwenye tamasha hilo’’,alisisitiza.

Tamasha la kitaifa la utamaduni lilianzishwa mwaka 2022 ikiwa ni kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan  aliyoyatoa alipokuwa mgeni rasmi mkoani Mwanza Septemba 8,2021 katika Tamasha la utamaduni la Bulabo.

Rais Samia aliagiza matamasha ya utamaduni kufanyika kwa mzunguko kila Mkoa ili watanzania wajue mila na desturi za kila Mkoa ambapo aliagiza kuwe na mashindano ya ngoma za asili na washindi wapewe Tuzo.

Malengo makuu ya tamasha la kitaifa la utamaduni ni kurithisha amali za utamaduni kwa vitendo, kuchochea maendeleo ya utalii wa kiutamaduni, Sanaa za

asili,sekta za ubunifu wa asili, kuhamasisha utaifa,uzalendo na urithishaji wa maadili kwa mtanzania

## SERIKALI YAWAKOMBOA WANANCHI WA MPITIMBI



Serikali imewaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya wananchi wa Kata ya Mpitimbi Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma baada ya kuboresha huduma za afya katika hospitali ya Halmashauri hiyo iliyojengwa Kijiji cha Mpitimbi.

Mbunge wa Jimbo la Peramiho ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Sera,Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa niaba ya wananchi wa Mpitimbi amemshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za kutekeleza mradi huo.

“Nainua sauti ya moyo wa shukrani kwa Rais Samia kwa sababu kata ya Mpitimbi haikuwahi kuwa na ndoto ya kujengewa hospitali kubwa ya Wilaya’’,alisema.

Amesema wananchi wa Kata ya Mpitimbi na Tarafa ya Muhukuru matibabu yao ya kibingwa ilikuwa ni lazima wayapate kwenye hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea au Kwenda kwenye hospitali ya Rufaa ya Misheni ya Mtakatifu Joseph Peramiho.

Amesema Jimbo la Peramiho lina kata saba katika Tarafa ya Muhukuru ambazo sasa zitakuwa zinapata huduma za matibabu katika hospitali ya Mpitimbi na kwamba hospitali hiyo pia inatoa huduma kwa wananchi wa nchi Jirani ya Msumbiji ambao wanapakana na Jimbo la Peramiho katika Kijiji cha Mkenda kilichopo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Amesema serikali imeboresha majengo na kununua vifaa tiba vya kisasa ambavyo vinawezesha huduma za matibabu za kibingwa kutolewa katika hospitali hiyo.

# BWAWA LA MPITIMBI  KIVUTIO KINGINE SONGEA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu  Mheshimiwa Jenista Mhagama ameagiza kuboreshwa Bwawa la maji la asili lililopo katika Kijiji cha Mpitimbi  wilayani Songea mkoani Ruvuma ili  liingizwe kwenye mpango  ufugaji endelevu  wa viumbemaji.

Waziri Mhagama amesema hayo wakati anazindua mradi wa kuimarisha lishe na ufugaji endelevu wa viumbemaji  kwa wakulima wadogo uliofanyika Kijiji cha Mpitimbi wilayani Songea.

Katika mradi huo serikali kupitia shirika la IFAD imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.1 kutekeleza mradi huo katika wilaya za Songea na Mbinga mkoani Ruvuma na Wilaya za Ruangwa na Mtama mkoani Lindi,mradi ambao unatekelezwa kwa miaka miwili kuanzia Machi 2024 hadi Machi 2026.

“kuna bwawa la Mungu linalovutia sana lipo  hapa Mpitimbi tena lipo njiani tu mnaweza kujionea ili kuangalia namna mnavyoweza kulitumia bwawa hilo la asili lenye ukubwa wa hekta 17  lenye uwezo wa kuingia samaki wengi kama litaboreshwa vizuri’’,alisisitiza Mhagama.

Mbunge huyo wa Peramiho amesema wamedhamiria kuiona Mpitimbi inakuwa kituo kikubwa cha ufugaji wa Samaki baada ya kuboresha bwawa hilo ambalo litakuwa kivutio kwa wawekezaji na chanzo kikubwa cha mapato na lishe bora kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma

Mhagama amesema Bwawa hilo ni kivutio kikubwa kwa wageni wengi pia linaweza kusaidia mradi huu wa ufugaji endelevu wa viumbemaji wakiwemo samaki ambapo Serikali ya Rais Samia imewekeza mabilioni ya fedha kutekeleza mradi huu.

## SERIKALI YABORESHA HOSPITALI YA TUNDURU




SERIKALI imetoa shilingi milioni 900 kufanya ukarabati majengo ya hospitali kongwe ya wilaya ya Tunduru mkoanI Ruvuma pamoja na kununua vifaa tiba hali ambayo imeboresha huduma za afya zinazotolewa katika hospitali hiyo.

# ROBO TATU YA WILAYA YA NAMTUMBO NI HIFADHI



Utafiti umebaini kuwa robo tatu ya wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ni hifadhi ikiwemo eneo la Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na ushoroba unayounganisha Selous na Niassa unaoanzia mkoani Ruvuma hadi nchini Msumbiji.

Kuna hifadhi tatu za jamii ndani ya Wilaya ya Namtumbo ambazo ni Mbarang'andu, Kisungule na Kimbanda.

Wilaya ya Namtumbo inahusika katika mradi mkubwa wa umeme wa bwawa la Nyerere katika Mto Rufiji unaoendelea kutekelezwa na serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Mto Luegu unaonzia Wilaya ya Namtumbo unachangia asilimia 19 ya maji katika Mto Rufiji hivyo Mkoa wa Ruvuma unahusika moja kwa moja na uendelevu wa mradi wa bwawa la Nyerere katika Mto Rufiji ambao umekusudia kuondoa mgawo wa umeme nchini.

Utalii wa uwindaji unaofanyika katika Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori ya Mbarang'andu wilayani Namtumbo imekuwa kivutio kikubwa cha watalii kutoka nchi za Ulaya na Marekani ambao wanatembelea jumuiya hiyo yenye vijiji saba na kufanya aina hiyo ya utalii ambayo inahusisha moja kwa moja matumizi ya wanyamapori.

Jumuiya hiyo inahusisha vijiji saba ambavyo ni Mchomolo, Kitanda, Likuyuseka Maganga, Kilmasela, Nambecha, Songambele na Mtelemwahi.

Afrikanus Challe ni Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma anasema utalii wa uwindaji unafanyika katika mapori ya akiba yaliyopo sehemu mbalimbali nchini na kwamba aina hiyo ya utalii inakwenda sanjari na utalii wa picha ambao ni utalii wa kutazama mandhari na kupiga picha bila kuhusisha uwindaji wa wanyama na kwamba utalii wa picha pia husisha matumizi ya moja kwa moja ya wanyamapori.

## WAZIRI NDUMBARO ALIVYOSIKILIZA KERO ZA WANANCHI



Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini Dkt. Damas Ndumbaro amekamilisha ziara ya kiserikali ya kutembelea kata zote 21 za Manispaa ya Songea.

Lengo kuu la ziara hiyo likiwa ni kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi .

Dkt.Ndumbaro alianza ziara hiyo kuanzia tarehe 09 Julai 2024 na kuhitimisha tarehe 17 Julai 2024.

Katika ziara hiyo Dkt. Ndumbaro aliambatana na Wataalamu mbalimbali kutoka Sekta ya Elimu, Afya, Mipango miji, Uchumi, Kilimo, Tasaf, TARURA, TANROAD,

SOUWASA, viongozi wa vyama vya Siasa, na Waheshimiwa Madiwani ambapo amefanikiwa kukamilisha kutembelea kata zote 21 za jimbo la Songea Mjini.

Miongoni mwa kero ambazo amesikiliza na kuzitafutia ufumbuzi ni changamoto ya miundombinu ya Barabara, Vivuko na mifereji, ukamilishaji wa miundominu ya ofisi za Serikali za mita, miundombinu ya elimu Msingi, umeme, na maji.

## SERIKALI YATOA BILIONI 1.77 KUJENGA SHULE MBINGA



Wananchi wa Kata ya Muungano iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wametoa eneo lenye ukubwa wa ekari 9.5 kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ambayo utekelezaji wake upo mbioni kuanza baada ya Halmashauri kupokea zaidi ya Shilingi bilioni 1.77 kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya Kata ya nyoni, Litembo, Muungano na nyumba ya mwalimu Kata ya Kitumbalomo.

Hayo yamebanishwa na Diwani wa Kata ya Muungano Mhe. Paulo Kayombo alipozungumza katika kikao cha kutambulisha mradi wa ujenzi wa shule hiyo kwa wananchi wa Kata hiyo kilichofanyika hivi karibuni..

“Sisi wananchi wa Kata hii tumetoa eneo ukubwa wa ekari 9.5 kudhihirisha kuwa tupo tayari kushirikiana na Serikali katika ujenzi huu,sambamba na eneo hili

tutashirikiana na Serikali bega kwa bega kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati na katika ubora” Amebainisha Mhe. Kayombo

Naye Diwani wa Kata ya Kitumbalomo Mhe. Denis Kapinga amebainisha kuwa wananchi wa Kata ya Kitumbalomo wameukubali mradi wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu ambayo utagharimu shilingi milioni 95 hadi kukamilika kwa kuwa mradi huo.

## WANANCHI MADABA WAASWA KUFUGA NYUKI



Mhifadhi wa shamba la miti Wino TFS katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma Groly Fotunatus ametoa rai kwa wananchi wa Madaba kujiunga katika vikundi ili waweze kupewa mizinga ya kufugia nyuki.

Mhifadhi huyo ametoa rai hyo katika hafla fupi ya kukabidhi vifaa mbalimbali vya ujenzi katika taasisi za kidini na Serikali kwa Mbunge wa Jimbo la Madaba Dkt.Joseph Mhagama.

Hata hivyo Mhifadhi huyo amewatahadharisha wananchi wahakikishe wanaacha kukata miti na kulima kilimo cha mabondeni badala yake wafuge nyuki.

“Undeni vikundi kupitia Halmashauri,pale ofisini kwangu kuna mizinga 30 inasubiri kikundi hivyo yote hya ni jitihada za kutunza mazingira'',alisisitiza.

## WANAFUNZI WAAHIDI KUFANYA VIZURI MTIHANI WA TAIFA



Wanafunzi wa Kidato cha tano na kidato cha sita Shule ya Sekondari Ruanda iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wameahidi kufanya vizuri katika mtihani wao wa kuhitimu kidato cha sita na kusisitiza kuwa wote watapata daraja la kwanza.

Ahadi hiyo imetolewa na Kaka Mkuu wa Sekondari ya Ruanda Oswin Saga alipozungumza kwa niaba ya wananafunzi katika kikao kilichofanyika shuleni hapo hivi karibuni

" Tumeona matokeo ya wenzetu wamefanya vizuri nikuahidi kiongozi kuwa tutashirikiana kwa pamoja na walimu tukizingatia nidhamu na masomo sisi ni divisheni I hayo madaraja mengine ni mwiko kwetu" Amebainisha Oswin

Kwa upande wake Mkuu wa shule hiyo mwalimu Paschal Kisese ameeleza kuwa matokeo yajayo yataleta faraja zaidi kwa kuwa ufaulu wa shule hiyo unapanda kila siku hivyo Serikali itegemee matokeo mazuri zaidi ya kidato cha sita kwa mwaka 2025 na kuendelea.

Naye Afisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Felix Danda amewapongeza walimu na wanafunzi kwa matokeo mazuri ya mtihani wa kidato cha sita yaliyotoka hivi karibuni ametoa rai kwao kuongeza juhudi na jitihada kufikia malengo waliyojiwekea.

Matokeo ya shule hiyo Kidato cha sita mwaka 2024 daraja la kwanza walipata wanafunzi 54 .

# WAZAZI WAHIMIZWA KUTOA MLO KAMILI KWA WATOTO



Katibu Tawala Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma Mtela Mwampamba amewahimiza wazazi na walezi kuwapa watoto vyakula vyenye mchangonyiko wa mlo kamili.

Mtela ameyasema hayo katika kijiji cha Mtepa Kata ya Lituta Halmashauri ya Madaba wakati wa zoezi la Utoaji wa vifaa mbali mbali vyenye thamani ya shilingi milioni 39 vilivyotolewa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika Shamba la miti Wino Madaba,

Mwampamba amesema licha ya wakazi wa Madaba kuwa na utajiri wa fedha wana changamoto ya kutozingatia mlo kamili ili kuepukana na udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Mhifadhi Mkuu wa shamba la miti Wino Groly kasmir amesema kuwa wametoa vifaa hivyo kwa shule za msingi,makanisa,na hospitali kwa lengo la kurejesha sehemu ya mapato kwa jamii .

Amesema wakazi hao wamekuwa Mstari wa mbele kusimamia hifadhi hiyo huku akiwataka kuendelea kuwa walinzi kwa watu ambao wamekua wakitorosha moto unaosababisha hasara kwa serikali na watu binafsi.

## WIZARA YA NISHATI YAKABIDHI GARI TANESCO MBINGA



Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga leo Julai 20, 2024 amekabidhi gari la kubebea nguzo katika Ofisi ya TANESCO Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma.

Wakati akikabidhi gari hilo Mhe. Kapinga amesema Serikali itaendelea kuboresha maslahi, vitendea kazi na mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wa TANESCO ili kuwapa motisha ya kuendelea kufanya kazi kwa bidii.

"Kulikuwa na changamoto ya kubeba nguzo kupeleka kwenye maeneo mnayofanyia kazi, Serikali inaamini magari haya yataleta tija na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi ikiwemo kutoa huduma kwa wakati kwa wateja." Amesema Kapinga

Akizungumzia changamoto ya kukatika kwa umeme wilayani Mbinga, Kapinga amesema Serikali imeshaweka mikakati ya kujenga kituo kipya cha umeme ambacho kitaboresha hali ya upatikaji umeme.

Ameongeza kuwa, kituo hicho cha kupokea na kupoza umeme kitajengwa katika mradi wa Gridi Imara Awamu ya Pili.

Amesema TANESCO inaendelea kuboresha miundombinu ya umeme

## UKUMBI WA KISASA WA SEKONDARI YA DKT.SAMIA NAMTUMBO



Ukumbi wa sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma inayoitwa Dkt Samia Suluhu Hassan wenye uwezo wa kuchukua watu 1,500.Sekondari hiyo yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 1,000 wa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita imejengwa eneo la Migelegele wilayani Namtumbo .Hadi sasa serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 4.45 kutekeleza mradi huo uliofikia zaidi ya asilimia 95 na tayari wanafunzi wameanza masomo .



## UKUMBI WA BWALO SEKONDARI YA SAMIA WAANZA KUTUMIKA



MBUNGE wa Jimbo la Namtumbo mkoani Ruvuma Mheshimiwa Vita Kawawa ameutumia ukumbi wa bwalo la chakula katika sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma ya Dkt.Samia Suluhu Hassan iliyojengwa eneo la Migelegele wilayani Namtumbo.

Mbunge ameutumia ukumbi huo kugawa majiko ya gesi 300 yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 25 ambayo ameyatoa kwa wajasirimali wadogo ili kuhakikisha wajasirimali hao wanatumia nishati safi kupikia.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan hadi sasa imetoa shilingi bilioni 4.45 kujenga sekondari hiyo ambayo hadi sasa ina wanafunzi 600 wanaosoma katika sekondari hiyo yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 1000 wanaosoma kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

# VIJIJI 84 NYASA VYAFIKIWA NA UMEME



Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga amezindua mradi wa umeme katika shule ya Sekondari ya Nyasa mjini Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma.

Akizungumza na wananchi wa wilaya ya Nyasa, katika Kata ya Chiwanda amesema amelazimika kufanya ziara mkoani Ruvuma, baada ya kuona Wilaya ya Nyasa na Mbinga miradi ya umeme wa REA, haijakamilika katika ngazi ya vijiji.

Amemuagiza Mkandarasi wa REA kukamilisha haraka miradi hiyo Ili serikali ianze kutekeleza miradi ya umeme katika ngazi ya vitongoji.

Aidha amesema katika Wilaya ya Nyasa huduma ya umeme tayari imefika katika vijiji 84.

Kwa upande wao wananchi wa wilaya ya Nyasa wameipongeza Serikali kwa kutatua changamoto ya Umeme katika Kata ya Chiwanda ambayo ipo mpakani mwa Nchi ya Tanzania na Msumbiji.

# NAIBU WAZIRI WA NISHATI AGAWA MITUNGI YA GESI 850 MBINGA




Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga kwa kushirikiana na Kampuni ya Gesi ya Oryx Tanzania amegawa jumla ya majiko ya mitungi ya gesi 850 yenye thamani ya shilingi milioni 76 kwa wananchi wa Wilaya ya Mbinga, Mkoa wa Ruvuma.

Ugawaji wa mitungi hiyo yenye unalenga kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kupitia Mkakati wa Taifa wa matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034), Serikali imedhamiria kuongeza kaya za watanzania zinazotumia nishati safi ya kupikia kutoka asilimia 10 ya sasa mpaka kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2034.

Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga amesema mpaka sasa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imesambaza mitungi ya gesi ya ruzuku 83,500 yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.5 bilioni.

Hata hivyo Naibu Waziri amesema katika mwaka huu wa fedha serikali imepanga kutoa mitungi ya gesi 452,445 yenye thamani ya Shilingi bilioni

# MBUNGE NAMTUMBO AKABIDHI GESI KWA WAJASIRIAMALI



Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Namtumbo mkoani Ruvuma Mheshimiwa Vita Kawawa akikabidhiwa majiko ya gesi ya Mwakilishi wa Mkurugenzi wa ORYX Tanzania Peter Ndomba ambapo Mbunge huyo ametoa majiko ya gesi 300 yenye thamani ya shilingi milioni 25 kwa wajasiriamali wadogo ili kuunga mkono kampeni ya matumizi ya nishati safi.

Hafla ya ugawaji wa majiko hayo ya gesi imefanywa na Mbunge huyo katika ukumbi wa sekondari ya wasichana ya Dkt Samia Suluhu Hassan eneo la Migelegele mjini Namtumbo.

## NAIBU WAZIRI AZINDUA MATUMIZI SAHIHI YA MBOLEA RUVUMA




MATUMIZI ya mbolea hapa nchini,yameongezeka kutoka wastani wa tani 363,599 katika msimu wa kilimo 2021/202 hadi kufikia tani 840,714 kwa msimu wa kilimo 2023/2024.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa mbolea Tanzania Joel Lauren amesema hayo jana,wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha usajili wa wakulima na matumizi sahihi ya mbolea uliofanyika wilayani Mbinga.

Amesema,Mkoa wa Ruvuma ambao ni kati ya Mikoa ya kimkakati ya uzalishaji wa chakula hapa nchini, kwa miaka ya karibuni umeongoza kwa matumizi ya mbolea ambapo msimu 2022/2023 Mkoa huo ulitumia zaidi ya tani 83,472.

“katika msimu 2023/2024 mkoa wa Ruvuma umetumia tani 100,000,hivyo kuendelea kuwa kinara kwa matumizi ya mbolea na kuwa miongoni mwa mikoa tegemezi katika uzalishaji wa chakula hapa nchini”amesema.

Laurent alitaja mikoa inayofuatia kwa matumizi ya mbolea ni Njombe tani 75,358,Mbeya tani 75,252,Songwe tani 71,230 na mkoa wa Iringa ambao umetumia tani 44,214.

Amesema,matumizi ya mbolea kwa sasa ni muhimu kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu kunakohitaji ongezeko la uzalishaji wa chakula ili kukidhi mahitaji,ukuaji wa miji,miundombinu na huduma za kijamii zinazochangia kupunguza eneo linalofaa kwa kilimo.

Ameeleza kuwa,matumizi sahihi ya mbolea kunaongeza tija na kuchangia kukuza kipato cha mkulima mmoja mmoja,ukuaji wa sekta ya kilimo na pato la Taifa kwa ujumla.

Ameongeza kuwa,hapa nchini kuna mbolea za viwandani na mbolea za asili ambazo zinatumiwa na wakulima,lakini changamoto ni matumizi kidogo ya mbolea kwa baadhi ya maeneo kunatokana na dhana potofu kwamba mbolea inaharibu ardhi na baadhi ya wakulima kukosa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea"alisema Laurent.

Amewakumbusha wakulima umuhimu wa kutumia mbolea katika uzalishaji wa mazao kwenye mashamba yao kwani unasaidia kurutubisha,kuboresha afya ya udongo na kuzalisha mazao kwa wingi katika eneo dogo.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nishati Mheshmiwa Judith Kapinga amesema,sekta ya kilimo ndiyo mhimili wa uchumi wa Tanzania na inaajiri takribani theluthi mbili ya nguvu kazi ya Taifa na inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwandani,asilimia 100 ya usalama wa chakula na zaidi ya asilimia 26 ya pato la Taifa.

Kapinga amesema,katika mazingira ambayo kilimo ndiyo sekta ya uchumi,maendeleo ya mwananchi na Taifa kwa ujumla yanategemea zaidi ufanisi katika sekta hiyo.

Amesema,Serikali ya awamu ya sita imedhamira kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya kilimo kwa kuongeza bajeti ya wizara kutoka takrbani Sh.bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Sh.trilioni 1.24 kwa mwaka 2024/2025.

Amewataka wakulima hapa nchini wakiwemo wa wilaya ya Mbinga na mkoa wa Ruvuma,kuchangamkia fursa zinazotolewa na Serikali kwa kujisajili katika mfumo wa kidijitali kupitia Ofisi za Watendaji wa vijiji na mitaa.

Naibu Waziri Kapinga amesema,kujisajili kwenye mfumo wa kidijitali kutawaweza wakulima kununua mbolea kwa gharama nafuu,kuongeza uzalishaji,kuboresha maisha yao na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Ametaja faida nyingne kwa wakulima kujisajili kwenye mfumo wa kidijitali,ni kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi zitakazotumika kuweka mipango ya kuwaendeleza wakulima,sekta ya kilimo na kupata huduma za ugani,taarifa za masoko na huduma za kifedha kupitia kanzidata.

Kaimu Katibu Tawala wa mkoa wa Ruvuma Jumanne Mankhoo,ameipongeza mamlaka ya udhibiti wa ubora wa mbolea kwa kusimamia vema upatikanaji wa pembejeo za ruzuku iliyosaidia kupatikana kwa wingi na kwa urahisi katika meneo mengi ya mkoa huo.

Naye Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja wa TFRA Dkt Louis Kasera amesema,kampeni hiyo inalenga kuhamasisha wakulima kote nchini juu ya matumizi sahihi ya mbolea ili waweze kongeza uzalishaji.

Amewahakikisha wakulima kuwa,mpango wa mbolea za ruzuku utaendelea kutolewa hadi katika msimu wa kilimo 2024/2025 na kuwataka wakulima waongeze juhudi na kutumia mbolea kwenye shughuli zao za kilimo.

## WAZIRI MKUU AWAAGIZA WAKUU WA MIKOA NA WILAYA KUSIMAMIA MIRADI



WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya wasimamie miradi yote ya maendeleo kwenye mikoa na wilaya zao na kuhakikisha inakamilishwa ili ianze kutoa huduma kwa wananchi.

“Kwenye eneo la usimamizi wa miradi, Wakuu wa Mikoa hakikisheni mnazo taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo; hii ni fursa yenu ya kujua benki tuliyonayo ya utekelezaji wa miradi yote ya tangu mwaka 2021. Angalieni ni miradi gani imepata fedha, na mjiridhishe kama imekamilika au la, na kama bado haijakamilika, fuatilieni ni kwa nini haijakamilika.”

Waziri Mkuu ametoa maagizo hayo wakati akizungumza na Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya Pamoja na viongozi wa CCM wa Mikoa kwenye kikao kazi

alichokiendesha kwa njia ya mitandao (video conference) kutokea ofisi ndogo ya Waziri Mkuu iliyoko Magogoni, jijini Dar es Salaam.

## BARABARA YA MBINGA -MBAMBABAY ILIVYOGEUKA KIVUTIO CHA UTALII



Barabara ya lami nzito inayounganisha wilaya za Mbinga hadi Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma yenye urefu wa kilometa 66 ambayo iliyogharimu zaidi ya shilingi bilioni 129 imegeuka kivutio cha utalii kwa wageni wengi wanaosafiri kupitia barabara hiyo.



# NYUMBA YA NYERERE NA SAMORA KIVUTIO CHA UTALII TUNDURU




ENEO la Masonya lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma lina utajiri wa utalii wa malikale na utambulisho wa Taifa, ingawa bado halifahamiki na wengi.

Eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 100 lina vivutio adimu vya utalii wa malikale ikiwemo nyumba yenye namba A 10 ambayo walikuwa wanafikia na kuishi Marais Hayati Julius Nyerere wa Tanzania na Hayati Samaro Machel wa Msumbiji kuanzia 1966 hadi mwaka 1975 wakati wa harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika.

Mhifadhi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Bartazar Nyamusya anasema viongozi hao pia wakiwa katika nyumba hiyo, walitumia jengo dogo maalum lililopo jirani ya nyumba hiyo kama chumba cha mawasiliano yote na nchi zilizokuwa katika harakati za ukombozi kusini mwa Afrika.

Moja ya mambo yanayovutia katika eneo la Masonya ni kwamba Rais wa sasa wa Msumbiji Mheshimiwa Filipe Nyusi akiwa na wazazi wake katika harakati za ukombozi wa nchi hiyo,alifika Masonya mwaka 1970 akiwa na miaka nane na kusoma katika shule ya msingi FRELIMO iliyokuwa katika Kata ya Masonya.

Mhifadhi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji anasema mwaka 1966 Tanzania iliwapokea wapigania uhuru wa Msumbiji na kuwakabidhi eneo la Masonya.

Hata hivyo anasema eneo hili limebaki kama eneo la makumbusho ambapo ametaja urithi unaopatikana katika eneo hilo kuwa ni nyumba mbili za viongozi wa kitaifa hayati Samora Machel Rais wa kwanza wa Msumbiji na Nyumba aliyokuwa anafikia baba wa Taifa hayati Mwl.Julius Nyerere.

Anautaja urithi mwingine kuwa ni ukumbi wa semina aliokuwa anatumia Samora Machel kutoa mafunzo mbalimbali na majengo 11 ambayo kwa sasa ni madarasa ya wanafunzi wa sekondari ya wasichana Masonya.

Maeneo mengine ya urithi ni mahandaki yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa Msumbiji,eneo la bendera ya FRELIMO na eneo la mnara ulipofanyika mkutano wa wanawake wa Msumbiji tarehe 17/3/1973 .

Mwaka 1975 baada ya nchi ya Msumbiji kupata uhuru wapigania uhuru hao walirudi katika nchi yao na kuanzia mwaka 1990 Halmashauri ya Tunduru iliamua kuanzisha shule ya sekondari ya wasichana Masonya yenye wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita.

Eneo la malikale la Masonya linatakiwa kuendelezwa kwa sababu linaweza kutoa mchango mkubwa katika nyanja za utalii, uchumi, elimu na utafiti.



## WANANCHI WAIOMBA SERIKALI NAMTUMBO IWE NA MAJIMBO MAWILI



MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma pichani kushoto Mheshimiwa Juma Pandu ameiomba Serikali kuona umuhimu wa kuligawa jimbo la Namtumbo ili wananchi waweze kupata huduma mbalimbali kwa urahisi tofauti na hivi sasa jimbo hilo lina kata 21 ambalo kijografia kata zake zimekaa mbali na makao makuu ya halmashauri hiyo ambalo linapakana na Wilaya ya Tunduru,Mkoa wa Morogoro na Nchi jirani ya msumbiji.

Pandu ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mkongo Nakawale amesema kuwa kwa ujumla hali ya wananchi ambao wanahitaji kupata huduma ya halmashauri wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa namna ya kufika makao makuu ya Halmashauri .

Amesema kuwa wakazi wa maeneo za Kata za Magazini na Lusewa ambazo zipo umbali wa kilomita Zaidi ya 280 hadi makao makuu ya Wilaya wamekuwa wakishindwa kusafiri au kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kwenye kata zao kutokana na umbali uliopo na miundombinu ya barabara hasa kipindi cha masika inakuwa mibovu.

Pandu amesema kutoka kata ya kitanda hadi makao makuu ya wilaya ya namtumbo kuna umbali wa Zaidi ya kilomita 150 jambo ambalo limekuwa likisababisha shughuli mbali mbali za maendeleo kuto tekelezwa kwa wakati kutokana na miundo mbinu ya barabara kuwa mibovu.

## FURSA NYINGINE YA UTALII KATIKA WILAYA YA NYASA



Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvumaimebarikiwa kuwa na fursa karibu zote za utalii ikiwemo utalii wa ikolojia na kiutamaduni ambapo hivi sasa imebainika kuna fursa nzuri ya kuona utalii wa kilimo hususan kupitia zao la Kahawa aina ya Arabica inayolimwa katika tarafa ya Mpepo wilayani humo.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya amesema kahawa inayolimwa wilayani Nyasa ina soko kubwa katika soko la Duniani kwa kuwa watumiaji wanapenda ladha na namna inavyonukia ukilinganishwa na kahawa zinazozalishwa katika maeneo mengine Duniani

## WANANCHI NAMTUMBO WAOMBA KUSOGEZEWA HUDUMA ZA KIBINGWA



WAKAZI wa wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma,wameiomba Serikali kuhakikisha huduma za kibingwa za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo zzinakua endelea ili kuwafikia wananchi wengi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini.

Wametoa ombi hilo ,wakati wa zoezi la uchunguzi na matibabu za magonjwa ya moyo zinazotolewa na wataalamu kutoka Taasisi ya tiba ya magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete(JKCI) katika Hospitali ya wilaya Namtumbo.

Said Ngonyani,ameomba serikali kupitia Taasisi hiyo kuwa na utaratibu ya kuwawekea kambi ya madaktari bingwa kama hao angalau mara moja kwa mwezi ili wananchi wengi waweze kupata huduma za kitabibu na kupunguza gharama za usafiri kufuata huduma hizo.

Ngonyani amesema,wananchi wengi wanaishi maeneo ya vijijini na vipato vyao ni vidogo na haviwezi kumudu gharama za kufuata huduma za kibingwa katika Hospitali za rufaa,hivyo wengi wao wanajukuta wakiathirika na kupoteza maisha kwa kukosa matibabu ya kibingwa.

Mkuu wa wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngollo Malenya,amewataka wananchi wa Namtumbo kujitokeza kwa wingi na kutumia fursa hiyo kwenda kupata vipimo na matibabu ya magonjwa ya moyo ili kuwa na afya itakayowawezesha kushiriki katika shughuli zao za maendeleo.

Malenya,amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa zaidi ya Sh.bilioni 1.5 kwa ajili ya uboreshaji wa vituo vya afya katika wilaya ya Namtumbo ikiwemo kituo cha afya Lusewa na Sh.bilioni 1.3 kwa ajili ya kununua vifaa tiba.

**WAGONJWA 496 NAMTUMBO WAGUNDULIKA NA PRESSURE**



WATU 496 sawa na asilimia 71 kati ya watu 696 waliofanyiwa uchunguzi wa awali wa magonjwa ya moyo kutoka vijiji mbalimbali katika wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, wamebainika kusumbuliwa na shinikizo la juu ya Damu.

Wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa chakula wenye uhusiano wa moja kwa moja na ugonjwa wa moyo ni asilimia 37na wagonjwa 222 sawa na asilimia 32 wamegundulika kuwa na matatizo ya kisukari.

Hayo yamesemwa na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete(JKCI) Dkt Baraka Ndelwa,wakati wa zoezi la awali la uchunguzi wa magonjwa ya moyo na shinikizo la damu lililofanyika katika kijiji cha Luhimbalilo kata ya Mputa wilayani Namtumbo.

Amesema,wametoa rufaa kwa wagonjwa watano kwenda Hospitali ya Jakaya Kikwete kwa uchunguzi zaidi na wagonjwa wengine wamewapa rufaa kwenda Hospitali ya Rufaa ya mkoa Songea (Homso)na Hospitali ya St Joseph Peramiho.

Dr. Ndelwa ameema,katika zoezi hilo wamegundua watu wengi wanaugua magonjwa ya moyo na sukari, lakini wanashindwa kupata matibabu ya uhakika kutokana na upatikanaji wa matibabu ya kwenye ngazi ya zahanati na vituo vya afya kutokuwa rafiki.

Amesema,ugonjwa wa shinikizo la damu husababisha matatizo mbalimbali ikiwemo kiharusi,na moyo kushindwa kufanya kazi hali inayoweza kusababisha kifo kwa mgonjwa ambaye hajapata matibabu.

Dkt Ndelwa,ameshauri kuanzishwa kliniki maalum za uchunguzi wa magonjwa ya moyo na shinikizo la damu kwenye vituo vya afya na Hospitali za wilaya, ili kuweza kuwafuatilia kwa karibu wananchi watakaobainika kupata ugonjwa huo,na kuwawezesha watoa huduma vifaa vya kisasa vya kutolea huduma kwa wagonjwa.

Ameiomba serikali,kupeleka dawa za magonjwa ya moyo na kisukari kwenye zahanati ili ziweze kuwasaidia wananchi wengi wenye matatizo hayo,badala ya kuishia kwenye Hospitali za rufaa za mkoa ambako upatikanaji wake ni rahisi.

## ASKARI WA TANAPA WAPIGA KAMBI TUNDURU



KIKOSI cha askari kutoka Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere kanda ya kusini kituo cha Kalulu,kimeweka kambi maalum katika kijiji cha Milonde wilayani Tunduru mkoani Ruvuma ili kusaidia kufukuza wanyama wakali na waharibifu hususani Tembo wanaotoka kwenye hifadhi na kuvamia makazi ya watu.

Askari hao watahusika kufukuza Tembo katika vijiji vya Changarawe, Namwinyu,Kajima,Kalulu,Milonde na Matemanga ambavyo vimekuwa na matukio ya wananchi kuvamiwa na Tembo mara kwa mara wakiwa katika shughuli zao.

Afisa Uhusiano wa Tanapa kituo cha Kalulu mkoani Ruvuma Stephen Mpondo amesema,kazi kubwa itakayofanywa na askari hao ni kuzuia Tembo kabla hawajafika kwenye mashamba ya wananchi na kuwarudisha kwenye maeneo yao.

Amesema,askari wataendelea kuwepo katika kijiji hicho kwa muda mrefu ili kuhakikisha wananchi wanabaki salama na wanaendelea na shughuli zao za uzalishaji mali hasa kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo.

Amewataka wananchi na viongozi wa vijiji hivyo,kuhakikisha wanatoa taarifa haraka mara tu wanyama wanapovamia kwenye mashamba yao kabla hawajafanya uharibifu wa kula mazao.

Mpondo amewaomba wananchi,kuwapa ushirikiano askari ili waweze kutekeleza majukumu yao hasa ikizingatia kufukuza Tembo au wanyama wengine hatari siyo jambo rahisi na jepesi kunahitaji watu wenye uthubutu na waliopata mafunzo ya namna ya kukabiliana na wanyama hao.

## KAYA ZAIDI YA 400 TUNDURU KUNUFAIKA NA UMWAGILIAJI



ZAIDI ya kaya 4,000 katika Halmashauri ya wilaya Tunduru mkoani Ruvuma,zinatarajia kunufaika na fursa ya kilimo cha umwagiliaji kupitia utekelezaji wa mradi wa skimu ya umwagiliaji ya Nambarapi iliyopo kata ya Masonya wilayani humo.

Mradi huo unaotekelezwa na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya umwagiliaji,utawanufaisha wakulima wanaolima mazao mbalimbali ikiwemo Mpunga,mahindi pamoja na mazao ya mboga mboga.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo Mhandisi wa umwagiliaji mkoa wa Ruvuma Lusia Chaula alisema,mradi utatekelezwa kwa muda wa siku 560 kuanzia tarehe 15 Julai 2024 na utakamilika tarehe 31 Disemba 2025.

Chaula amezitaja gharama za mradi ni Sh.6,314,477,066.00 na utajengwa kwa kumtumia Mkandarasi kampuni ya M/S Company Ltd JV Otendo ambapo zaidi ya ekari 1,700 zimetengwa kutumika kwenye mradi huo.

Kwa mujibu wa Chaula, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa banio na tuta,ujenzi wa mfereji mkuu mita 5,975,ujenzi wa mfereji wa upili mita 8,825,kujenga mfereji wa matupio,ujenzi wa barabara za mashamba,ujenzi wa vivusha maji na ofisi ya Mhandisi wa mradi

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Tunduru Chiza Marando amesema,haijawahi kutokea katika wilaya hiyo kuwa na mradi wa umwagiliaji wenye thamani kubwa tangu wilaya ilipoanzishwa.

Marando amesema,mradi wa skimu ya umwagiliaji Nambarapi unakwenda kutoa uhakika wa chakula na kupatikana kwa ajira za muda kwa vijana wengi wanaotoka katika kata ya Masonya na wilaya ya Tunduru kwa ujumla.

“kupitia mradi huu tuna mhakikishia Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwamba,wilaya ya Tunduru tutaendelea kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha na uhakika wa chakula ambacho kinaweza kutosheleza mahitaji ya wananchi wetu”alisema.

Mkuu wa wilaya ya Tunduru Simon Chacha,amemtaka mkandarasi kuhakikisha anatekeleza mradi huo haraka na kwa viwango kama ilivyo kwenye makubaliano yaliyopo katika mkataba.

Chacha,amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazofanya za kuleta maendeleo katika wilaya ya Tunduru ikiwemo kutoa zaidi ya Sh.bilioni 6.3 fedha ambazo zitatumika kutekeleza mradi huo wa umwagiliaji utakaowanufaisha wananchi wengi hususani wakulima wa wilaya ya Tunduru.

## WAFANYABIASHARA WA MAZAO MBINGA WATAHADHARISHWA




Wafanyabiashara wa mazao Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wametakiwa kufuata taratibu zilizopo wakati wa kusafirisha mazao ili kuepuka usumbufu pamoja na adhabu ya kulipa faini pindi watakapokiuka taratibu zilizopo.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura alipozungumza na wafanyabiashara hao ofisjni kwake

" kuna baadhi ya wafanyabiashara hawafuati sheria zilizopo wakati wa kusafirisha mazao kuna baadhi hata leseni zimepita muda wake sasa ili tuweze kwenda sawa lazima tufuate taratibu zilizowekwa",alisema.

Aidha amewataka wafanyabiashara hao kuendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa kutoa taarifa pindi wanapogundua wafanyabiashara ambao wanakiuka taratibu hatua ambayo itapelekea kudhibiti upotevu wa mapato.

## MILIONI 120 ZA MAPATO YA NDANI MBINGA ZAJENGA WODI TATU



Mkurugenzi wa Idara ya Afya Ustawi wa Jamii na Lishe Ofisi ya Rais-TAMISEMI Dkt. Rashid Mfaume amempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura kwa kutenga fedha Shilingi Mil. 120 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa wodi tatu ( wanaume, wanawake, watoto) zinazojengwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Dkt. Mfaume ametoa pongezi hizo katika ziara ya ufatiliaji na usimamizi shirikishi iliyofanywa na timu ya wataalam kutoka OR-TAMISEMI kukagua utoaji wa huduma katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga

## WATUMISHI WAPYA 675 RUVUMA HAWAJAFANYIWA UPEKUZI



Mkaguzi Mkuu wa Nje kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi CPA Deogratias Waijaha amesema watumishi wapya 675 kutoka Halmashauri za wilaya ya Mbinga,Nyasa na Mbinga mji mkoani Ruvuma hawajafanyiwa upekuzi ili wakae sawa kwenye utumishi wa umma.

CPA Waijaha amesema hayo wakati anazungumza kwa nyakati tofauti katika kikao maalum cha Baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) juu ya hoja na mapendekezo CAG kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 katika Halmashauri hizo.

Mkaguzi Mkuu huyo amebainisha kuwa kati ya watumishi hao watumishi 369 wameajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga,watumishi 225, Halmashauri ya Nyasa na watumishi 81 wa Halmashauri ya Mji Mbinga ambapo ameagiza watumishi hao kufanyiwa upekuzi ili wakidhi sifa ya utumishi wa umma.

Hata hivyo Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma zimepata Hati Safi katika ukaguzi wa CAG uliofanywa katika mwaka 2022/2023.

## TUNDURU YAPATA HATI SAFI KWA MIAKA MITANO MFULULIZO



Halmashauri ya wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma imeendelea kupata hati safi kwa miaka mitano mfululizo.

Hayo yamesemwa katika kikao maalum cha Baraza la madiwani cha kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa hesabu za serikali pamoja na hoja za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

kikao hicho kilichofanyika kwenye ukumbi wa Sky way mjini Tunduru kimehudhuriwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed

# KAHAWA INANAYOVUTIA ZAIDI DUNIANI IPO WILAYA YA NYASA



WIlaya Nyasa mkoani Ruvuma imebarikiwa kuwa vitu adimu ambapo kahawa aina ya arabica inayolimwa katika Tarafa ya Mpepo wilayani Nyasa mkoani Ruvuma imebainika ndiyo kahawa inayovutia na kunukia zaidi katika viwango vya kahawa kwenye soko la Dunia.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya anawaalika wageni mbalimbali kwenda kufanya utalii wa kuona kahawa hiyo inayopendwa zaidi katika soko la nje ambayo inalimwa kwenye safu za milima ya Umatengo.

Nyasa ndiyo wilaya pekee mkoani Ruvuma ambayo ardhi yake ina rutuba ya kutosha hivyo kustawisha mazao karibu yote bila kutumia mbolea ya kemikali

## SIRI YA HALMASHAURI ZOTE RUVUMA KUPATA HATI SAFI



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge amemshukuru Mkaguzi Mkuu wa Nje kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi CPA Deogratias Waijaha kwa maelekezo aliyokuwa anayatoa kwenye ukaguzi hali iliyosababisha Halmashauri zote nane mkoani Ruvuma kupata Hati Safi.

Madenge ametoa shukurani hizo wakati anazungumza katika kikao maalum cha Baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) juu ya hoja na mapendekezo CAG kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma amemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanalı Ahmed Abbas Ahmed kwenye Kikao hicho.

## MBINGA VIJIJINI YAONGOZA UKUSANYAJI MAPATO RUVUMA



Mkuu wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma Mheshimiwa Kisare Makori ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa kukusanya mapato kwa asilimia 110 na kuweza kupata Hati Safi.

Makori ametoa pongezi hizo wakati anatoa salamu za Wilaya katika kikao maalum cha Baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) juu ya hoja na mapendekezo CAG kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.



## MADABA YAJIVUNIA HATI SAFI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameipongeza Halmashauri ya Madaba kwa kupata Hati safi ikiwa ni matokeo ya Ukaguzi ambao ulifanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Kanalı Abbas ametoa pongezi hizo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge katika kikao maalum cha Baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) juu ya hoja na mapendekezo CAG kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kwa Halmashauri ya

Madaba

## MUONEKANO WA KITUO CHA AFYA KIHAGARA



Hiki ni kituo cha Afya Kata ya Kihagara wilayani Nyasa mkoani Ruvuma ambacho kimekuwa mkombozi mkubwa kwa wanancni wa mwambao mwa ziwa Nyasa na baadhi ya wananchi kutoka wilayani Kyela mkoani Mbeya wanafika kutibiwa katika kituo hicho cha Afya.



## WILAYA YA NYASA KITOVU CHA UTALII MKOA WA RUVUMA



Mbunge wa Jimbo la Nyasa mkoani Ruvuma Mhandisi Stella Manyanya akizungumza na wananchi wa kata ya kihagara ambao walishiriki katika tamasha la utamaduni na mila ambalo hufanyika kila mwaka mwezi Julai ambapo vikundi nane vya ngoma ya mganda vilivyopo katika kata hiyo vilionesha burudani nzito



Eneo linaloitwa Bustani ya mawe mwambao mwa ziwa Nyasa katika kata ya Kihagara wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma imekuwa moja ya kivutio cha utalii

## KAYA ZAIDI YA 18,000 ZAHITIMU MPANGO WA TASAF RUVUMA



Jumla ya kaya 18,912 zimehitimu mpango wa kunusuru kaya masikini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Mkoa wa Ruvuma.

Hayo yamesemwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge wakati anazungumza kwenye kikao kazi cha waratibu wa TASAF,wahasibu wa TASAF na maafisa ufuatiliaji wa Mkoa wa Ruvuma kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mipango ofisi ya Mkuu wa Mkoa mjini Songea.

Amesema hadi kufikia Juni 2024 Mkoa wa Ruvuma ulikuwa na Jumla ya kaya 65,089 za walengwa wa TASAF katika vijiji 685.

Hata hivyo amezitaja kaya ambazo zitaendelea na mpango wa TASAF katika Mkoa wa Ruvuma kuwa ni kaya 46,177.

## RC RUVUMA AAGIZA UDHIBITI UPOTEVU WA FEDHA KWENYE HALMASHAURI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewaagiza waheshimiwa madiwani na wataalam kuhakikisha wanadhibiti upotevu wa fedha kwa kuchukua hatua kwa wanaosabisha upotevu huo.

Kanali Abbas ametoa agizo hilo wakati anazungumza katika kikao maalum cha Baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) juu ya hoja na mapendekezo CAG kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea



## MFUMO WA M-MAMA SASA KUSHUKA HADI NGAZI YA JAMII




Serikali kupitia Wizara ya Afya imetoa mafunzo ya mfumo wa M-MMA kwa Maafisa Habari na Watoa Elimu ya Afya kwa Umma ngazi ya Halmashauri ili kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na Wajawazito na Watoto Wachanga katika jamii.

Akizungumza wakati kufunga mafunzo hayo Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr. lious Chomboko amewataka Washiriki kwenda kuyafanyia kazi kwa umakini mafunzo hayo kwa lengo la kutimiza adhima ya Serikali ya kuokoa maisha ya Wajawazito na Watoto Wachanga.

Chomboko amesema lengo la serikali ni kuona idadi ya vifo vya Wajawazito na Watoto Wachanga katika jamini hivyo waende kusimamia na kutoa elimu zaidi katika jamii kutumia elimu waliyopata katika mafunzo hayo.

## RC RUVUMA AWAKABIDHI MAGARI MAPYA WAKUU WA WILAYA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewakabidhi wakuu wa Wilaya watatu magari mapya ya kisasa yaliyonunuliwa na serikali.

Hafla ya kukabidhi magari hayo imefanyika kwenye viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa mjini Songea ambapo wakuu wa Wilaya za Tunduru,Mbinga na Namtumbo wamekabidhiwa magari hayo.

Akizungumza kabla ya kukabidhi magari hayo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma amemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa uwezeshaji mkubwa wa fedha uliosababisha kupatikana kwa vifaa vya usafiri ambavyo vinakwenda kutumika na wakuu wa Wilaya.

Amesema kwa kuanzia serikali ilitenga bajeti ya kununua magari mapya kwa wakuu wa wilaya watatu ambao walikuwa na changamoto kubwa ya magari ambapo amewatia moyo wakuu wa wilaya ambao hawajapata magari mapya kuwataka wawe na Subira kwa kuwa serikali itaendelea kutenga bajeti ya ,kununua magari.

“Magari haya yamenunuliwa kwa fedha nyingi,hivyo thamani ya fedha inatakiwa kuakisi thamani ya fedha iliyotumika kwa kuwahudumia wananchi kwenye maeneo yao,wananchi wanatamani kuona changamoto zinazowakabili zinatatuliwa’’,alisisitiza.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngollo Malenya akizungumza kwenye hafla hiyo,amempongeza Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za kununulia magari kwa wakuu wa wilaya za Mkoa wa Ruvuma.

Amesema ukosefu wa magari kilikuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wakuu wa wilaya ambapo iliwalazimu wakati mwingine kuazima magari kwa wakuu wa Idara ili Kwenda kutatu changamoto kwa wananchi.

Awali Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge aliyataja magari mapya yaliyonunuliwa na serikali kuwa ni gari lenye namba STN 2928 ambalo limenunuliwa kwa ajili ya Mkuu wa Wilaya ya Tunduru,gari STN 2929 kwa ajili ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga na STN 2927 kwa ajili ya Wilaya ya Namtumbo.

Madenge amesema magari hayo yatawasaidia wakuu wa Wilaya hizo kutekeleza majukumu yao ya kila siku ya ufuatiliaji na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi




## MKOA WA RUVUMA WAPATA TUZO NYINGINE



Mkoa wa Ruvuma umeshinda Tuzo ya Mkoa unaoongoza kuwa na mazao Mengi zaidi Tanzania yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Akizungumza wakati anamkabidhi Tuzo hiyo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma,Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Ruvuma Peja Muhoja amesema Tuzo hiyo ya kitaifa imetolewa mjini Tabora kwenye maadhimisho ya siku ya Ushirika Duniani ambapo Tuzo mbalimbali zilitolewa

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo ofisini kwake mjini Songea,amewapongeza wakulima wa Mkoa wa Ruvuma ambao wamekubali kuuza mazao yako kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo amewashauri wakulima wengine katika maeneo mbalimbali kuhakikisha wanauza mazao yao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ,mfumo ambao ameutaja kuwa na manufaa makubwa kwa wakulima ikiwemo kuuza mazao kwa bei kubwa.

## KISIWA CHA PUULU KILIVYOSHEHENI VIVUTIO VYA UTALII



Hiki ni kisiwa cha Puulu ziwa Nyasa wiayani Nyasa mkoani Ruvuma.Kisiwa hiki kipo Kata ya Liuli kutoka katika fukwe za Puulu hadi ndani ya kisiwa kwa boti ni umbali wa dakika tatu .kisiwa hiki kina vivutio mbalimbali ikiwemo msitu wenye miti ya asili ambayo ni kijani wakati wote,

kuna makazi ya ndege adimu duniani wakiwemo ndege aina ya ngwazi wenye uwezo wa kuvua samaki,pia kisiwa hiki ni makazi ya ndege aina ya kanga na samaki watamu wa aina mbalimbali wanazaliana kando kando mwa kisiwa cha Puulu.Kisiwa hiki ni sehemu tulivu ya kupumzika kikiwa ha hali ya ubaridi wakati wote na upepo mwanana kutoka katika ziwa Nyasa.

## BILIONI 2.5 ZAJENGA HOSPITALI MBINGA VIJIJINI



Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa zaidi ya shilingi bilioni 2.5 kutekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma.Hospitali hiyo imeanza kutoa huduma muhimu za afya kwa wananchi

## HOSPITALI YA NAMTUMBO KUCHUNGUZA MAGONJWA YA MOYO



TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete inatarajia kuitumia Hospitali ya wilaya Namtumbo kama kituo kidogo cha uchunguzi wa Matibabu ya moyo ili kusaidia wananchi wenye hali ya chini mkoani Ruvuma kupata huduma karibu za matibabu.

Madaktari Bingwa kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete(JKCI) wamepiga kambi ya siku saba wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma kwa ajili ya kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo kwa wananchi wa wilaya ya Namtumbo.
Akizindua huduma hizo Mbunge wa Jimbo la Namtumbo Mheshimiwa Vita Kawawa amesema, zoezi la uchunguzi na matibabu ya moyo kwa wananchi litasaidia kuokoa maisha ya watu wengi ambao awali walishindwa kupata huduma hizo kutokana na gharama ya kufuata matibabu nje ya wilaya ya Namtumbo.

Kawawa,ameishukuru Serikali kupitia Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete(JKCI),kwa kuleta Madaktari Bingwa watakaotoa huduma kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na magonjwa ya moyo,uzito mkubwa na shinikizo la damu.

Aidha Kawawa,ameipongeza serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuleta zaidi ya Sh.bilioni 2.3 zilizosaidia kuboresha miundombinu ya Afya katika Hospitali ya wilaya Namtumbo. Amesema,fedha hizo zimetumika kujenga jengo la huduma za meno, macho,jengo la mama ngojea na jengo la Mama,Baba na mtoto.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa wilaya ya Namtumbo Dkt Aaron Hyera amesema,uboresha wa miundombinu katika sekta ya afya uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita umesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati na baada ya kujifungua.

Amesema uwekezaji wa miundombinu katika sekta ya afya wilayani humo umewezesha kutoa huduma kwa ubora zaidi hasa ikizingatiwa baadhi ya vijiji viko umbali wa zaidi ya kilometa 200 kutoka makao makuu ya wilaya Namtumbo mjini na vituo vya afya vilivyopo.

## MUONEKANO WA HOSPITALI YA WILAYA YA NYASA



Muonekano wa hospitali ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma ambayo inatoa hudumu zote muhimu kwa wananchi wa Mbambabay na wilaya ya ya Nyasa kwa ujumla.Kabla ya hospitali hiyo wananchi wa wilaya ya Nyasa walikuwa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

## BILIONI 3.7 ZILIVYOJENGA MAJENGO 16 HOSPITALI YA MADABA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya shilingi bilioni 3.7 kujenga majengo 16 katika hospitali ya Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo Dr.Wambura Chacha amesema hata hivyo hospitali hiyo inahitaji majengo 31 ambapo amesema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma mbalimbali kulingana na hatua ya ujenzi na vifaa tiba vilivyopo.

Amezitaja huduma ambazo zimeanza kutolewa katika hospitali hiyo kuwa huduma za afya za wagonjwa wa nje, huduma ya kliniki ya mama,baba na mtoto na huduma ya dharura na kwamba wanasubiri vifaa kutoka serikali kuu ili hospitali hiyo iweze kuanza kutoa huduma za afya zinazilingana na hadhi ya hospitali ya wilaya.

## UTAMADUNI UNAVYOCHOCHEA MAENDELEO RUVUMA



UTALII wa kiutamaduni bado ni nadharia changa katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, kwa kuwa nchi hizo zimezoea kuona utalii wa ikolojia.

Utalii wa ikolojia ni kuona vitu vya asili kama kutembelea mbuga za wanyamapori, ndege, wadudu, milima, mabonde, misitu, maporomoko, mito, maziwa, mapango na chemchem.

Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Balthazar Nyamusya anavitaja vivutio vya utalii wa kiutamaduni kuwa ni majengo ya makumbusho, historia, ngoma za asili, nyimbo za asili, lugha, michezo ya jadi, sanaa, vinyago, matamasha, vyakula, kilimo na mavazi.

Utalii wa kiutamaduni ni nadharia mpya hapa nchini ambapo serikali imeanza kuutambua utalii wa kiutamaduni na kuupa nguvu kubwa aina hiyo ya utalii ambayo inaweza kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya utalii hapa nchini.

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa michache nchini yenye fursa lukuki za utalii wa kiutamaduni na utalii wa ikolojia ambazo hadi sasa wananchi wamefaidika kwa kiwango kidogo kutokana na sekta hiyo kutopewa kipaumbele katika mkoa huo.

Ili kuhakikisha utalii wa kiutamaduni unachochea maendeleo, serikali ya Awamu ya Sita imeamua kuanzisha tamasha la kitaifa la utamaduni ambalo mwaka huu linafanyika mkoani Ruvuma kuanzia Julai 20 hadi 27 mwaka huu.

Tamasha la kitaifa la utamaduni lilianzishwa mwaka 2022 ikiwa ni kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa alipokuwa mgeni rasmi mkoani Mwanza Septemba 8,2021 katika Tamasha la utamaduni la Bulabo.

Rais Samia aliagiza matamasha ya utamaduni kufanyika kwa mzunguko kila Mkoa ili watanzania wajue mila na desturi za kila Mkoa ambapo aliagiza kuwe na mashindano ya ngoma za asili na washindi wapewe Tuzo.

Malengo makuu ya tamasha la kitaifa la utamaduni ni kurithisha amali za utamaduni kwa vitendo, kuchochea maendeleo ya utalii wa kiutamaduni, Sanaa za asili,sekta za ubunifu wa asili, kuhamasisha utaifa,uzalendo na urithishaji wa maadili kwa mtanzania

Vivutio vya utalii wa kiutamaduni vilivyopo katika Mkoa wa Ruvuma ni majengo ya kihistoria, makanisa, makumbusho ya vita vya Majimaji, historia ya machifu, jiwe la Mbuji, mapango ya wamatengo na pango la mlima Chandamali lililokuwa maficho ya chifu Songea Mbano wakati wa vita ya Majimaji.

Siku za nyuma vivutio vya utalii wa kiutamduni kama vile majengo ya kale,maeneo ya kihistoria na makumbusho hayakupewa mtazamo wa kiuchumi zaidi.Mhadhili Msaidizi kutoka Idara ya Utalii wa Kiutamaduni Frank Kimaro anasema Maeneo hayo yalipewa mtazamo wa kielimu zaidi na kuundwa Idara za Mambo ya Kale na Idara ya Makumbusho ya Taifa.

Mabadiliko duniani ndiyo yaliyosukuma kuwepo kwa utalii wa kiutamduni na nchi zilianza kutoa kipaumbele katika utalii wa kiutamaduni ndiyo maana hapa nchini Idara za Mambo ya kale na Makumbusho zilihamishwa kutoka Wizara ya Elimu na kuingia katika Wizara ya Utalii na Maliasili.

Mabadiliko ya utalii wa kiutamaduni hayawezi kuonekana kwa haraka badala yake inatakiwa watalaamu kuwahamasisha wananchi kutambua fursa zilizopo katika aina hiyo ya utalii na kuzitumia ipasavyo fursa zilizopo ili kujiletea maendeleo yao binafsi na Taifa kwa ujumla wake.

Ni vigumu kutenganisha utalii wa ikolojia na utalii wa kiutamduni kutokana na aina hizo mbili za utalii kuwa na mahusiano ya karibu,Watalii wanapoingia nchini wote wanavutika na utalii wa aina zote mbili.

Mtalii anapokwenda kutembelea utalii wa ikolojia kama mbuga za wanyama pia anaweza kupita katika maeneo yenye utalii wa kiutamaduni na kwamba fursa ya utalii wa kiutamaduni ni kubwa kwa wananchi wa kawaida kuliko aina nyingine za utalii.

Utalii wa kiutamaduni unazungumzia jamii husika na kwamba jamii hiyo inaweza kufaidika kutokana na utalii wa kiutamaduni ambao unapatikana katika eneo husika hadi kufikia ngazi ya kitaifa.

Unaweza kuona aina hii ya utalii ni tofauti na utalii wa ikolojia ambao tunaangalia zaidi mbuga za wanyama na maeneo ya asili ambayo yametengwa na serikali ambapo wahusika wakubwa ni serikali yenyewe na siyo watu binafsi, katika utalii wa kiutamaduni wahusika wakuu ni  wananchi wenyewe .

Wananchi katika utalii wa utamaduni wanaweza kunufaika kuanzia kiwango cha familia, mtaa, kitongoji, kijiji, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa hiyo utalii wa kiutamaduni unatoa fursa kubwa ya ukuaji wa uchumi kuanzia kwa mtu binafsi hadi kwa taifa.

Hata hivyo inaelezwa kuwa licha ya utalii wa utamaduni kuonekana kumlenga zaidi mwananchi wa kawaida, lakini kipato anachopata mwananchi huyo kwa kucheza ngoma au kuuza bidhaa za jadi na kazi nyingine za mikono kipato chake kimekuwa cha chini na kuwakatisha tamaa.

Vitu anavyovifanya mwananchi katika utalii wa kiutamaduni vina thamani kubwa kuliko mapato anayopata na kwamba katika hali ya kawaida vitu vya utamaduni vina thamani kubwa na vikiachwa kupotea haviwezi kupatikana tena kwa kuwa hakuna kiwango cha malipo kamili kwa shughuli za utalii wa kiutamaduni.

Utafiti umebaini kuwa utalii wa kiutamaduni unaweza kubadilisha kiwango cha maisha ya watu kutokana na kupata kipato kinachoweza kuwaongezea kipato cha ziada katika mapato yao.

Bidhaa zinazotokana na utalii wa kiutamaduni kama samani zilizotengenezwa kwa miti na sanamu za kuchonga zimekuwa zinauzwa na watu binafsi kwa watalii na wageni wengine kwa bei za juu kwa mfano kiti kinachotengezwa kwa kutumia miti ya mianzi kinauzwa kati ya sh. 200,000 hadi 400,000.

Nafasi ya utalii wa kiutamaduni ni kubwa katika kukuza uchumi wa nchi, utalii unachangia uchumi wa Tanzania katika kiwango kikubwa  na kuchukua nafasi ya pili hivyo utalii endelevu una nafasi kubwa katika kuleta maendeleo endelevu.

Soko la vitu vya utamaduni wa kitalii vinatoa ajira kwa watu wengi wakiwemo mwenye duka, mtengenezaji na msambazaji hivyo kufungua fursa za ajira za moja kwa moja kwa wananchi ambapo watu wengine wananufaika na utalii wa utamaduni kutoka kwenye migongo ya watu walioajiriwa moja kwa moja katika sekta hiyo.

Kuna nchi nyingi ambazo zimekuza uchumi wake kwa haraka kupitia utalii wa kiutamaduni zikiwemo Australia, Ujerumani, Uingereza na nchi nyingine za ulaya ambazo kutokana na ukosefu wa mbuga za wanyama wengi kama zilivyo katika Afrika wameamua kuendeleza utalii wa kiutamaduni zaidi kuliko utalii wa asili na kupata maendeleo makubwa kupitia aina hiyo ya utalii.

## HIFADHI YA GESIMASOA MADABA YENYE MAZALIA YA SAMAKI ADIMU DUNIANI



Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo imebarikiwa kwa kuwa na neema ya vivutio lukuki na adimu vya utalii wa ikolojia na kiutamaduni.

Hifadhi ya Gesimasoa yenye ukubwa wa kilometa za mraba zaidi ya 700 ambayo ipo katika Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea,ni miongoni mwa vivutio adimu vya utalii.

Hifadhi hiyo ilianzishwa kama msitu wa hifadhi mwaka 1975 na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wa zamani Hayati Dk.Lawrence Gama mwaka 1975.Hatimaye mwaka 2015,Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma katika kipindi hicho hayati Said Mwambungu alisimamia mchakato wa kupandisha hadhi msitu huo na kuwa hifadhi ya Taifa.

Moja ya vivutio vilivyopo katika hifadhi hii ni mapumziko ya ndege maarufu duniani wanazaliana katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo iliyopo Makete mkoani Njombe wanaitwa kitaalam Derhams wenye uwezo wa kuruka toka bara moja hadi bara jingine.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anabainisha kuwa ndege hao wanapumzika hapa kwa miezi kadhaa kisha wanaendelea na safari

kupitia Bonde la ufa hadi ziwa Nyasa hatimaye wanasafiri hadi nchini Afrika ya Kusini mabara mengine.

Kulingana na Challe,hifadhi ya Gesimasoa ni mapito ya ndege hao ambao wanatoka Kaskazini mwa Afrika kuelekea Afrika ya Kusini ambao wanafuata milima ya Livingstone iliyopo ziwa Nyasa na kwamba ndege hao pia wanapumzika Mwambao mwa ziwa Nyasa hasa katika eneo la Kihagara ambapo kuna mazingira ambayo yanavutia ndege hao kuishi.

Kwa mujibu wa Challe,Hifadhi ya Gesimasoa pia ina mfumo wa ikolojia wa pori la Selous kwa sababu ni mapitio ya wanyamapori wanaotoka katika Pori la Akiba la Selous wanapita kuelekea Bonde la ziwa Nyasa kupitia pori la Liparamba hadi Hifadhi ya Niasa nchini Msumbiji ambapo wanyama wanakwenda nchini Msumbiji na kurudi Tanzania.

Wanyama ambao unaweza kuwaona katika hifadhi ya Gesimasoa ni tembo, simba,ndege, nyati, pofu na samaki adimu duniani aina ya mbelele na mbasa.

Hifadhi hii pia ni maingiliano ya mito miwili ya Hanga na Lutukira ambayo inatengeneza mto Ruhuhu unaomwaga maji yake ziwa Nyasa. Mto huo ndiyo mazalia ya samaki aina ya mbelele na mbasa ambao katika duniani nzima wanapatikana ziwa Nyasa pekee.

“Samaki hawa ni adimu sana kwa sababu utafiti umebaini samaki hawa wanapatikana ziwa Nyasa pekee na  wanazaliana katika mto Ruhuhu ambao unachangia asilimia 20 ya maji katika ziwa Nyasa’’,anasema Challe.

Utafiti wa samaki aina mbasa na mbelele katika mto Ruhuhu na ziwa Nyasa ulifanywa na Fransis Challe mwaka 2010 ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kitivo cha Sayansi,Teknolojia na Mazingira na chapisho la utafiti huo lilitolewa mwaka 2011.

“Samaki wanazaliana hapa kwenye Maingilio ya mito,kisha wanasafiri hadi ziwa Nyasa na kuendelea na maisha ambapo wakati wa kuzaliana samaki hao wanarudi tena hapa.Hivyo hili ni eneo muhimu sana kitaifa na kimataifa katika Uhifadhi na utalii kwa kuwa samaki hao hawapatikani sehemu nyingine yoyote Duniani’’,anasisitiza Challe.

Kwa mujibu wa Mhifadhi huyo hivi sasa wanyamapori wanahama toka Hifadhi ya Taifa ya Nyerere,wakipitia hifadhi ya Gesimasoa,hifadhi ya Litumbandyosi, Liparamba na kuvuka mpaka hadi hifadhi ya Niassa nchini.

## TABIA YA SOKWE INAFANANA NA BINADAMU KWA ASILIMIA 98



Utafiti umeonesha kuwa, asilimia zaidi ya 96 ya chembe za urithi za binadamu zinafanana na zile za sokwe, pia ubongo wa sokwe na vitendo vyao vinafanana sana na vile vya binadamu.

Profesa Richard wa somo la viumbe kutoka Chuo Kikuu cha Harvard nchini Marekani anaeleza kuwa, sokwe ni daraja pekee kati ya binadamu na maumbile hivyo ni vema wanyama hao kulindwa kwa nguvu zote.

Mhifadhi wa Hifadhi za Taifa,Noelia Mnyonga anasisitiza tafiti za kisayansi zimethibitisha kuwa Sokwe ni wanyama ambao wanafanana na binadamu katika tabia kwa asilimia 98 na kusisitiza kuwa ndiyo maana wanaitwa sokwe mtu.

“Sokwemtu ni mnyama ambaye alibakiza asilimia mbili tu angeweza kufanana na binadamu kitabia kwa asilimia 100 hali ambayo inamfanya mnyama huyu kutafutwa kwa udi na uvumba baada ya kuwa kivutio adimu na cha kipekee cha utalii duniani kote’’,anasema Mnyonga.

Mnyonga anasisitiza kuwa sokwe mtu ni mnyama wa ajabu ambaye kwa tabia na matendo hatofautiani sana na binadamu ndiyo maana baadhi ya watu wanamuita binadamu pori.

Sokwe mtu ni mnyama ambaye ni mfano halisi wa binadamu, mnyama huyu anavutia macho ya watalii wengi,ambao wanamiminika hapa nchini katika hifadhi ya Taifa ya Gombe mkoani Kigoms kwenda kuwashangaa wanyama hao adimu na wa aina yake.

Tafiti za kisanyansi zinaonesha kuwa sehemu ya ubongo wa sokwe inafanana na sehemu ya ubongo wa binadamu,hali hiyo ndiyo imesababisha sokwemtu kufanya matendo mengi ambayo yanafanywa na binadamu kwa mfano sokwemtu anaweza kupiga mswaki,kula chakula na kucheza kama binadamu.

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**


**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**
**SIMU Nambari.025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL:** ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**TOVUTI:www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; rs ruvuma**
**FACEBOOK: rs ruvuma**
**YOUTUBE:rs ruvuma**